www.ippmedia.com
Alasiri Online
Jumanne Februari 19, 2019 Tanzani 500/- Kenya 50/-



# SHILOLE
## RAIS MAGUFULI AMENISAIDIA KUJENGA NYUMBA



# SHILOLE

## RAIS MAGUFULI AMENISAIDIA KUJENGA NYUMBA

Na Anaeli Mbise

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Zuwena Mohamed maarufu kama Shilole amefunguka na kueleza kuwa mojawapo ya watu waliosaidia kukamilika kwa ujenzi wa nyumba yake ni Rais John Magufuli.

Akizungumza na Alasiri Online, Shilole amesema kuwa moja kati ya pesa alizopata na kuziwekeza katika ujenzi wa nyumba hiyo, zilitokana na kampeni za urais mwaka 2015 wakati wakimnadi mgombea wa Chama cha Mapinduzi (CCM), John Magufuli ambaye aliyeibuka mshindi wa kiti cha urais.

"Nyumba yangu imejengwa na muziki pamoja na kampeni za kumnadi Rais Magufuli, maana tulikuwa tunalipwa na tulilipwa pesa nyingi ndipo niliamua kuwekeza kwenye nyumba yangu," alisema Shilole.

Shilole aliongeza kuwa aliamua kununua kiwanja eneo la Majohe jijini Dar es asalaam na kuanza ujenzi mara moja tofauti na ilivyo kwa wanamuziki wengine ambao waliishia kununua magari na kufanya starehe.

Shilole ni miongoni mwa wasanii wa kike waliofanikiwa kumiliki nyumba kubwa na amesema kuwa aliijenga



# ROMA AELEZA KILA KITU KUHUSU 'ROSTAM'

Na Anaeli Mbise

BAADA ya tetesi kuzagaa kwenye mitandao ya kijamii zikidai kuwa kundi la Rostam limesambaratika, mmoja wa mwanamuziki anayeunda kundi hilo, Ibrahim Musa 'Roma Mkatoliki' ameweka wazi ukweli wa taarifa hizo.

Kundi la Rostam liliundwa mwaka 2017 na linajumuisha wasanii wawili ambao ni Stamina na Roma, na kutengeneza jina la Rostam.

Akizungumza na Alasiri Online kuhusu tetesi hizo, Roma alisema tetesi hizo hazina ukweli wowote na kwamba kazi zao zinaendelea kama kawaida.

"Makundi mengi huvunjika kwa sababu ya mambo mawili, pesa na wanawake, lakini bahati kwenye mabinti, mimi na Stamina tumefanikiwa hatupo huko na kwenye pesa pia tuko sawa. Rostam hatutavunjika hata kidogo," alisema Roma.

Kwa upande wake, Stamina alisema kuwa kundi hilo lipo imara na kuwataka mashabiki wao kuwa na subira kwani wanatarajia kuachia ngoma kali.

Tetesi za kuvunjika kwa kundi la Rostam zilishika kasi baada ya Roma kuachia wimbo wa kolabo na Billnass unaojulikana kwa jina la Funga Geti.

# Navy Kenzo waushika mtandao wa You Tube

Na Mary Kadoke

KUNDI la Navy Kenzo linaoundwa na wanandoa wawili, Emmanuel Mkono 'Nahreel' na Aika Marealle wameachia ngoma mpya iitwayo 'Roll it' ambayo imeanza kubamba katika mtandao wa You Tube.

Ngoma hiyo iliyotoka hivi karibuni imekuwa ikipendwa na mashabiki wengi katika mtandao huo, ambapo hadi juzi ilikuwa imeshaangaliwa na watazamaji 110,000 katika mtandao huo.

Mojawapo ya mashairi yaliyokuwapo katika wimbo huo unasema: "We only want to play on the weekends, roll it roll it girl we only want to play on the weekends"

Ngoma hiyo imeongozwa na Justin Campos na sauti kupikwa na Buskilaz.

Kundi hilo limewahi kutamba na ngoma mbalimbali ambapo kwa mwaka jana ngoma ya 'Katika' waliyomshirikisha msanii Diamond Platnumz iliwapa umarufu zaidi, ambapo ilitazamwa na watu milioni 11 kwenye mtandao huo wa You Tube.



# Dogo Janja amtaja mke wake mpya

Na Mary Kadoke

HATIMAYE msanii wa muziki wa kizazi kipya, Abdulaziz Chende maarufu Dogo Janja amethibitisha kupata mke mpya, baada ya kuachana na Irene Uwoya.

Kupitia kwenye ukurasa wake wa kijamii wa Instagram, Dogo Janja aliposti picha ya kimahaba akiwa na mke wake mpya, Queen Lina huku akimpamba na maneno matamu akiwa anamtakia heri ya siku ya kuzaliwa kwake.

"Hakuna neno linaloweza kutosha katika kuielezea furaha niliyonayo kwenye kufurahia siku yako ya kuzaliwa mpenzi wangu, Mengine nitakuelezea chumbani, kula ushibe kisha kaza chaga nakupenda sana," aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram @dogojanjatz.

Alasiri Online lilimtafuta Dogo Janja kuelezea kwa undani kuhusu posti hiyo, hata hivyo alisema hawezi kuzungumzia suala hili kwa sasa.



Dogo Janja alifunga ndoa na msanii wa filamu Irene Uwoya Oktoba 28, 2017 baada ya Uwoya kubadili dini kutoka kwenye Ukristo na kuwa Muislamu.

Hata hivyo, ndoa hiyo Iliingia katika misukosuko baada ya taarifa kuzuka na kudai kuwa Uwoya amepata mwanaume mwingine 'mchepuko' anayemuhudumia huku picha na video kuzagaa kwenye mitandao ya kijamii ikiwaonesha wakila raha jijini Dubai.

# DIAMOND
## AMTUMIA UJUMBE MZITO MPENZI WAKE



Na Mary Kadoke

MKURUGENZI wa nembo ya Wasafi Classic Bereau (WCB), Diamond Platnumz amemtumia ujumbe wa kimahaba mpenzi wake Tanasha Don, kwa kumweleza ataheshimu penzi lake maishani.

Diamond alimtumia ujumbe huo Tanasha kwenye ukurasa wake wa mtandao wa Istagram @diamondplatnumz ikiwa ni siku ya wapendanao duniani 'Valentine day' na kumsihi kupokea zawadi aliyotakuwa kupokea muda wowote akiwa nchini Kenya.

Sehemu ya andiko hilo lilisomeka kuwa "Kwa sababu wewe ni Valentine wangu wa milele, ni matumaini yangu kwamba utapokea surprise yangu ndogo, pamoja na umbali kututenganisha, kaa ukijua kuwa moyo wangu upo kwa ajili yako,"

Hata hivyo, Natasha alimjibu Diamond kwa kusema "Asante mpenzi wangi najiona mwanamke mwenye bahati duniani kuwa na wewe, maneno hayatoshi kuelezea jinsi gani ninavyojisikia kwa sasa."

Diamond ambaye kwa sasa anatamba kwenye wimbo alioshirikishwa na Rayvanny uitwao Tetetema ameingia kwenye mahusiano mapya na Tanasha ambaye ni raia wa Kenya.

Kabla ya kuwa na Natasha, Diamond alikuwa kwenye mahusiano na Zarina Hassan, na walipata watoto wawili, Latiffa Platnumz (3) na Nillan (2).

Nembo ya (WCB) inaundwa na wasanii mbalimbali kama vile Rayvanny, Harmonize, Mboso, Queen Darleen na Lavalava.

# MARTHA MWAIPAJA AWEKA WAZI MAHUSIANO YAKE

Na Anaeli Mbise

MWANAMUZIKI wa nyimbo za Injili nchini, Martha Mwaipaja amekanusha taarifa zilizopo katika mitandao ya kijamii zinazoeleza ameachana na mume wake, kwa kusema siyo kweli.

Amesema ataweka wazi kuhusu ukweli wa taarifa hizo muda ukifika, lakini mashabiki wake waelewe kuwa hajaachana na mume wake.

Martha aliyasema hayo wakati akizungumza na Alasiri Online, na kueleza kuwa kila jambo atalizungumza kwa muda wake kwa sababu muda ndiyo kila kitu na ukifika ataweka wazi ili watu waelewe.

"Kila jambo na majira yake, suala la mimi kutalakiana na mume wangu ntaliweka wazi muda ukifika, kwasasa siko tayari," alisema Martha.

Martha aliongeza kuwa kila mwanadamu anakutana na vitu tofauti katika maisha, na maandiko yanachukia talaka, hivyo inategemea katika maisha ya ndoa unapitia kitu gani au aina gani ya maisha.

Martha kwa sasa anatamba na nyimbo kama vile Sipiganagi Mwenyewe, Ni Siku Kuu, Nalifurahi, pamoja na Chakutumaini.

